

Swahili transcript:

Happy: Leo tunaonyesha mavazi ya kitanzania. Msichana wa kitanzania, m-dada, m-mama, anaweza akavaa mavazi kama haya. Hii ni t-shirt, na ina..unaona ina urembo wa shangashanga, hizi zinaitwa ni shanga. Na pia imeandikwa –*Beauty of Tanzania*; kuonyesha kwamba hii ni mali halisi ya Tanzania. Na pia, unaweza ukavaa na kitu kinachoitwa kikoi. Hiki ni kikoi; kimetengenezwa na..ni kama khanga, lakini yenyewe imetengenezwa kwa material tofauti. Na pia inakuwa kama imechanwakanwa huku pembeni ili kuongeza urembo. Na pia kinakuwa kinaweza kikawa na prints, prints tofauti kama hii mnaona kina za rangi ya brown; kama hizi ni mask yaani zimetengenezwa. Zote hizi zinaonyosha kwamba, yaani ni kama uafrikaafrika fulani. Halafu, pia tuna bangili kama hizi, kwa kingereza wanaita–bangles. Hizi ni bangles ambazo zimetengenezwa na magome ya miti, na mara nyingi zinavalika kama urembo. Kwa hiyo, unaweza ukavaa zako bangili yako, na pia unaweza ukavaa pete. Na hii hapa ni hina. Hina ni majani Fulani unatengeneza, unachukua unakuwa unayaponda; halafu unaweka na chai, unapaka, unaonekana kama ni urembo. Ni kitu ambacho ni asilia, sio kama rangi; hizi tunaziita nail polish. Yenyewe ni kitu tu asilia. Unapaka kwenye kucha, unaonekana kwamba mmh ! ni mwafrika halisi. Na pia tuna pete, hizi pete pia zimetengenezwa...ukiangalia kwa mfano pete hii hapa, utaona kabisa hii pete ni imetengenezwa na prints kama za chui ; tunamwita tiger. Halafu, ukiangalia pete hii, imetengenezwa na prints kama za zebra, za pundamilia. Unaona ina nyeupe na nyeusi ambayo inaweza ikawakilisha mali..mali ambazo tunazo, aah! maliasili tuseme; mbuga za wanyama ambazo kuna wanyama kama hawa. Kwa hiyo hii pia ina-symbolize kitu kuhusu Tanzania, vile vitu ambavyo tunavyo. Halafu pia, tuna shanga kama hizi hapa, ambazo tunazivaa kwenye miguu. Hii ni shanga ya mguuni, ambayo ni kama urembo tu. Imetengenezwa na nalii..shanga mbalimbali, kwa hiyo unavaa. Pia na hizi ni sandals, ambazo ni mali halisi ya Tanzania. Zimetengenezwa na hizi shanga ambazo zinataka kufanana na hizi. Pia ni flat, na ziko zinavutiaga sana watalii. Watalii wakifika, wanapenda sana kununua sandals kama hizi ambazo wengine wanaziita za kimasai. Kwa

hiyo, hii pia ni mkufu ambao umetengenezwa na magome ya miti, kama ambavyo imetengenezwa hii bangili. Kwa hiyo, huu mkufu pia umetengenezwa kwa magome ya miti. Halafu ukija hapa, tuna hereni; hereni ambayo pia imetengenezwa na gome la miti, ambayo ni mali halisi ya Tanzania. Hata ukiangalia printed zake zimetengenezwa kama vile...unaona kabisa yaani hiki kitu kimekaa, ni true african product. Pia ukiangalia, inafanana kidogo na hii bangle yangu ambayo pia imetengenezwa na gome la miti. Hii imetengenezwa sanasana na kifuu cha nazi. Nazi ni kitu ambacho tunatumia katika, ambayo wenyewe wanaita coconut; kwa hiyo hii ni kama imetoka kutoka kwenye *coconut tree*. Kwa hiyo, huyu ndiye msichana halisi wa kitanzania. Na pia unaweza ukaona hata nyuma ya hii nguo imekaa, hivi vidude vimeendelea kuwa huku. Na pembeni, kikoi chako ukikivaa, lazima hii, huu urembo huu ukae huku pembeni, unafunga kama unavyofunga khanga. Asanteni.

English translation:

Happy: Today we will show Tanzanian dresses. Tanzanian woman can wear many kinds of dresses. This is a T-shirt, and it has been decorated by beads. Also it reads “Beauty of Tanzania” to show that this is real product from Tanzania. You can wear a T-shirt with kikoi. This is *kikoi*, it is like *kanga* but this was made by different material. It has a fringe on all sides to add to the decorations. *Kikoi* can have prints. This one has brown prints.

These are masks which represent African culture. We also have bangles as they are called in English. These bangles have been made from tree shells, and people wear them as decorations. So you can wear bangles and a ring. This is called *hina*. *Hina* is a kind of leaf. People pound them and add them to tea, and then they apply them to their nails. It is a natural nail polish which makes you look truly African. Also we have rings. For example, this one is decorated with tiger prints, and this one is decorated with zebra prints. They portray the natural resources we have in Tanzania, such as the national parks where these kinds of animals are found. They symbolize what we have in Tanzania.

We also have beads which we wear on our legs. As you can see here, I have worn this type of bead. It is just for decoration and beauty.

These sandals are made in Tanzania. They are made by using beads which match these beads. The sandals are flat, and they are attractive to tourists visiting Tanzania. Tourists love to buy these sandals. Some people call these sandals “Maasai” sandals, because most Maasai people wear this kind of sandal. It is their tradition.

This is a necklace which has been made from tree shells. These are earrings made in Tanzania from tree shells. Its prints show true African products. These earrings match this bangle. This bangle was made from a coconut tree. So it is true that a Tanzanian woman, who wears a *kikoi*, makes sure that these decorations represent true African products. You wear *kikoi* much as you would wrap *kanga*.

Thank you!

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated